**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P. 38**
**GEITA**
**Simu: 028-2520004**
**Nukushi: (028) 2520040**
**Baruapepe:** rbcgeita@pccb.go.tz
**Website**: www.pccb.go.tz

**GEITA – JULAI 16, 2020.**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

## TAKUKURU MKOA WA GEITA YAOKOA JUMLA YA SHILINGI 230,318,570/=

**NDUGU WANAHABARI**
Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia kibali cha kukutana siku ya leo. Aidha ninawashukuru ninyi kwa kuitikia wito kuja kushiriki mkutano huu kwa ajili ya kuuhabarisha umma juu ya kazi ambazo zimetekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni, 2020. Karibuni sana ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita.

**NDUGU WANAHABARI**
Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 tumeweza kutekeleza majukumu ya TAKUKURU kupitia Uchunguzi na Mashtaka,Uelimishaji umma juu ya Mapambano dhidi ya Rushwa,Uzuiaji Rushwa na Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

**NDUGU WANAHABARI**
***Uchunguzi na Mashtaka wa tuhuma za Rushwa*** umewezesha uokoaji wa fedha jumla ya shilingi **230,318,570/=** zilizofanyiwa ubadhirifu kwa njia nyinginezo za Rushwa.

- Kiasi taslimu cha shilingi **171,227,131/=** ni fedha zilizorejeshwa kutokana na uchunguzi katika vyama vya ushirika kwa mchanganuo ufuatao;
  - Shilingi **83,088,631/=** zimetokana na uchunguzi tuhuma za ubadhirifu katika chama cha Ushirika Nyamatagata, Shilingi **44,100,000/=** za chama cha Ushirika wachimbaji wadogo wadogo cha Ikuzi wilayani Bukombe, shilingi **15,292,300/=** za chama cha

kuweka na kukopa cha Geita SACCOS, shilingi **7,118,200/=** ni za wakulima wa pamba katika AMCOS nne za Nyamzumula,Nyakasulwa,Katoma na Tupendane wilayani Geita na shilingi **21,628,000/=** ni za wakulima wa Pamba wilayani Mbogwe.

- Kiasi cha shilingi **21,457,667/=** ni fedha za CSR zilizolipwa kwa Wakandarasi kwa kazi hewa katika mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana Nyankumbu.

- Kiasi cha shilingi **8,800,000/=** ni fedha za manunuzi hewa katika mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Kinsabe wilayani Chato.

- Kiasi cha shilingi **6,785,000/=** zimetokana na malipo hewa katika zoezi la chanjo ya Surua Rubella mwaka 2014.

-Shilingi **10,000,000/=** ni sehemu ya fedha zilizolipwa na mkandarasi FAMOYO Construction Ltd wa mradi wa maji Nyamtukuza wilayani Nyang'hwale bila kuzifanyia kazi.

-Shilingi **700,000/=** ni fedha za malipo ya mishahara hewa katika Halmashauri ya wilaya Geita.

-Shilingi **622,000/=** ni za michango ya wananchi katika ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Nundu wilayani Nyang'hwale.

-Shilingi **4,670,772** ni fedha za ruzuku (capitation) kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu shule ya msingi Miembeni wilayani Chato zilizohusishwa na manunuzi hewa.

-Shilingi **1,516,000/=** ni fedha za malipo ya vibarua na mafundi katika mradi wa ujenzi wa madarasa shule ya sekondari Lulembela wilayani Mbogwe.

-Shilingi **400,000/=** ni fedha zilizotokana na mikataba ya udanganyifu katika biashara ya madini.
-Shilingi **4,140,000/=** ni fedha za faini kwa raia wa kigeni (wachina) waliokuwa wanaishi nchini nje ya muda wa vibali vyao vya kuwepo nchini.

Katika kipindi hiki cha Aprili hadi Juni pamoja na fedha zilizookolewa mikononi mwa mafisadi hawa Taasisi imeweza kufungua mashauri kumi (10) mahakamani ambapo jumla ya washtakiwa 17 ikiwa watumishi wa umma 11 na binafsi 06 wanaendelea kujibu mashtaka yao.Jumla ya mashauri yaliyoendeshwa mahakamani ni 35 ambapo 2 yalitolewa maamuzi na Jamhuri kushinda.

Aidha katika kipindi husika jumla ya malalamiko dhidi ya rushwa na makosa mengine 109 yamepokelewa na kinara wa kulalamikiwa ni sekta ya serikali za mitaa malalamiko 25,Kilimo 13, Madini 11, Ardhi 09, Ujenzi 08, Fedha 08, Elimu 07, Mahakama 06, Afya 04, Siasa 04, Polisi 03, Sekta binafsi 03, Biashara 03, Maji 02, Habari 01, Utamaduni 01,Uvuvi 01 na Ushirika 01.

Uchunguzi wa awali wa malalamiko haya umefanyika ambapo jumla ya majalada ya uchunguzi 11 yamefunguliwa, taarifa 12 zimehamishiwa idara nyingine, taarifa 37 zilitolewa ushauri na hatua za kiutawala na taarifa 49 zinaendelea kufanyiwa kazi. Katika kipindi hicho jumla ya majalada 11 uchunguzi wake umekamilika.

**NDUGU WANAHABARI**

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni TAKUKURU mkoa wa Geita imetekeleza jukumu la ***kuhamasisha umma kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa*** kwani bila ushiriki wa dhati wa jamii nzima mapambano haya hayataleta tija iliyokusudiwa.

Tumeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuelimisha kupitia semina 09, mikutano ya hadhara 10 ikiwa ni sehemu ya kuelimisha wananchi kuchagua viongozi bora na sheria ya uchaguzi katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu 2020 pamoja na elimu ya kampeni ya UTATU, VUNJA UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO na matumizi ya TAKUKURU APP, ufunguaji wa vilabu vya wapinga Rushwa katika vyuo 04, taarifa kwa vyombo vya habari 01, onesho 01, uandishi wa makala 08, mkutano na waandishi wa habari 01 na kugawa machapisho mbalimbali kwa wananchi.

**NDUGU WANAHABARI**

Kama nilivyoeleza awali kuwa majukumu mengine yaliyotekelezwa ni ***Uzuiaji Rushwa na Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo***.Katika uzuiaji rushwa lengo kubwa ni kufanya uchambuzi mifumo ya utendaji kazi ili kuziba mianya ya Rushwa kupitia warsha na matekelezo.

Katika kipindi hiki uchambuzi wa mifumo imefanyika sita (06) katika sekta za fedha,Manunuzi ya umma,Ushirika, Elimu, Nishati (REA) na Afya.

Kupitia uchambuzi hizo zilizofanyika tulibaini kuwepo kwa udanganyifu na ukiukwaji wa taratibu kwenye ukusanyaji wa mapato,manunuzi,matumizi ya fedha za elimu bure (capitation grands); wakulima kutolipwa fedha za mauzo ya mazao yao kwa wakati;

vifaa vya umeme kutokuwa na kiwango pia ubora uliotakiwa na vitendo vya rushwa kwenye utoaji na upatikanaji wa huduma za afya.

Kufuatia mapungufu haya ofisi imechukua jukumu la kuzishauri idara husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa na udanganyifu.

Aidha miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi **3,894,745,041/=** imefuatiliwa katika sekta za Afya, Elimu, Maji, Ujenzi na Nishati lengo likiwa ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia thamani ya fedha (value for money).

Miradi iliyofuatiliwa ni ujenzi wa: shule ya sekondari Nyalwanzaja (Geita), maboma ya madarasa katika shule ya msingi Katandalala (Mbogwe), mabweni mawili na bwalo la chakula katika shule ya msingi Nyakasaluma (Mbogwe), hostel shule ya sekondari Mwingiro (Nyang'hwale), ukamilishaji wa madarasa 19 katika shule za sekondari 09 (Nyang'hwale), madarasa shule ya msingi Nyijundu (Nyang'hwale),nyumba ya mwalimu shule ya msingi Beya (Nyang'hwale); ujenzi wa miundo mbinu ya maji Nyakagwe (Geita); ujenzi wa barabara ya lami km 02 katika mji wa Bukombe (Bukombe); ujenzi wa kituo cha afya (Namonge) na mradi wa ugawaji na usambazaji wa umeme wa REA (Chato).

Ufuatiliaji huo ulibaini changamoto ya miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi.

Aidha ofisi imechukua jukumu la kufanya warsha na wadau kuhusu manunuzi ya umma na usimamizi wa miradi pia kuzingatia taratibu na miongozo inayotolewa na watoa fedha.

## NDUGU WANAHABARI

## KUELEKEA UCHAGUZI MKUU 2020.

Sote tunafahamu kuwa mwaka huu mwezi Oktoba, 2020 tutakuwa na Uchaguzi Mkuu, uchaguzi huu unapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa, uhuru na demokrasia viweze kustawi, kuendelezwa na kudumishwa.

Ni vyema watanzania wakatambua kuwa uchaguzi ni fursa ambayo wanaitumia kutafakari mustakabali wa maendeleo ya maeneo yao na Taifa,ni fursa kuainisha changamoto zote zinazowakabili kama jamii kwenye maeneo yao kama vile barabara,maji,zahanati na ni fursa ya kutathimini uwezo wa viongozi waliochaguliwa katika uchaguzi uliopita

endapo walikuwa na mchango wowote katika kuwaletea maendeleo waliyotarajia.

Pia watanzania watambue kuwa lengo la uchaguzi ni kupata kiongozi mwadilifu, mwaminifu, uzoefu wa eneo la uchaguzi analogombea, awe na dira ya kuongoza, mchukia rushwa kwa maneno na vitendo na anayezingatia utii wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.Vile vile watambue thamani ya kura kuwa ni MAENDELEO, AMANI, UTULIVU na HAKI.

Aidha wananchi watambue kuwa wananchi wapokea na watoaji Rushwa hawawezi kuhoji masuala mbalimbali ya maendeleo kwa viongozi wao. Kwa kuzingatia umuhimu wa uchaguzi TAKUKURU tumejizatiti kufuatilia kwa umakini hatua kwa hatua uchaguzi huu, watakaojihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**NDUGU WANAHABARI**

Jukumu la kupambana na Rushwa ni letu sote mkiwemo ninyi. Mnaombwa kusaidia kufichua wagombea watoa rushwa kwa kutoa taarifa Takukuru kwani mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu letu sote. Vyombo vya habari ninaomba mtumie fursa mliyo nayo ya kuifikia jamii kwa kuwaelimisha kupitia vyombo vyenu kutambua thamani na umuhimu wa kura zao katika kupata viongozi walio bora.

**MWISHO**

Mikakati ya TAKUKURU Mkoa wa Geita kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2020 ni kuendelea kutatua kero za wananchi zinazohusiana na vitendo vya Rushwa, kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi ili waelewe haki na wajibu wao katika kuchagua viongozi bora katika uchaguzi mkuu 2020, kupata huduma, kuendelea kuwaelimisha watumishi wa sekta za Umma na binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wito wetu kwa wananchi wa mkoa wa Geita waendelee kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kuwa waadilifu kwa kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, washiriki pia kutoa taarifa za vitendo vya rushwa TAKUKURU kwa kupiga simu ya bure 113, *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au kupitia TAKUKURU APP.

**Sote Tuseme *"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**IMETOLEWA NA:**
**Leonidas R. Felix**
**MKUU WA TAKUKURU (M) GEITA**